



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE



Tarehe: 05/05/2023

Namba ya Kotesheni: LGA/071/2022/2023/RDC/W/39

KWA AJILI YA UTOAJI WA HUDUMA YA UFUNDI WA UJENZI WA BWENI LA
WANAFUNZI 80, MADARASA MAWILI NA CHOO CHA MATUNDU MATATU –
BARRICK PROGRAMME

MWALIKO WA KOTESHENI

Kwa:

.....

.....

1. Serikali ya Tanzania kupitia Ufadhili wa BARRICK GOLD TANZANIA imetenga fedha kwa ajili ya Ujenzi wa Miundo mbinu mbalimbali ya Shule za Sekondari nchini ambapo kwa Halmashauri ya Rungwe tumetengewa fedha katika **Shule ya Sekondari Tukuyu** kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Inakusudiwa kuwa sehemu ya fedha hizo zitatumika kugharamia malipo halali chini ya mkataba ambao unatolewa katika Mwaliko wa Kotesheni (MK).
2. Unakaribishwa kuwasilisha Kotesheni (Bei) kwa ajili ya utoaji huduma ya Ujenzi wa Miundo mbinu mbalimbali katika Shule hiyo kama ilivyoelekezwa kwenye Maelekezo ya Mahitaji na Bei kama ilivyofafanuliwa katika **Sehemu ya Pili. Miundo mbinu ya Shule** inayotarajiwa kujengwa katika **Shule ya Sekondari Tukuyu** ni Ujenzi wa **Bweni la Wanafunzi 80, Madarasa mawili (2) na choo cha matundu matatu (3) ya vyoo.**
3. Kufuatia fursa iliyotolewa hapo juu, Mkurugenzi Mtendaji (W) anawakaribisha mafundi ujenzi (Local Fundis)/Wakandarasi wenye sifa katika fani za Ufundi Uashi, Ufundi Seremala, Ufundi Aluminium na Ufundi Uchomeleaji (Grill) mwenye sifa zifuatazo:-

- Awe na elimu ya ufundi Uashi/ujenzi kutoka Vyuo vya Ufundi vinavyotambuliwa na Serikali na mwenye uwezo wa kujua kusoma ramani za majengo
- Awe na Namba ya Utambulisho wa mlipa Kodi (TIN Number)
- Awe na uwezo wa kutosha wa kifedha (kwa hiyo awasilishe Bank Statement)
- Awe na mafundi wasaidizi wenye ujuzi wa kujenga, kusuka nondo kwenye rinta, usukaji wa mifumo ya umeme, Mifumo ya maji safi na taka na kupiga rangi kwa unadhifu wa hali ya juu.
- Awe na uwezo wa kutengeneza madirisha ya Aluminium na milango ya alco bond).
- Awe na uwezo wa kutengeneza milango ya mbao ngumu
- Awe na uwezo wa kutengeneza milango ya "grill"
- Awe amewahi kufanya kazi ya ujenzi katika majengo ya Serikali au kwenye makampuni.

Nyaraka za maelezo ya zabuni kwa ajili ya mafundi kujaza kotesheni za ufundi husika zinapatikana katika ofisi ya **Mkuu wa Shule, Shule ya Sekondari Tukuyu S.L.P 148, Tukuyu.**

Kotesheni zote zilizojazwa kikamilifu kwa kuainisha Namba ya Kotesheni **LGA/071/2022/2023/RDC/W/39** zinatakiwa kuwasilishwa kwa **Mkuu wa Shule, Shule ya Sekondari Tukuyu S.L.P 148, Tukuyu** yakiwa yamefungwa vizuri kwenye bahasha nyuma ya bahasha ikitaja jina la kazi inayoombwa na Shule husika na kitalu husika.

Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha Kotesheni ni siku ya Alhamisi ya Tarehe 11/05/2023 kabla ya saa 5:00 Asubuhi. Kisha baada ya muda mfupi Kotesheni zitafunguliwa kwa uwazi mbele ya Mafundi walioomba kazi tajwa hapo juu.

Kotesheni ambazo hazitawasilishwa kabla ya muda uliotolewa hapo juu hazitakubaliwa wala kuzingatiwa kwa ajili ya tathmini bila kujali mazingira yoyote yale.

Wako katika ujenzi wa Taifa

Mchau, R.B

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE
 MKURUGENZI MTENDAJI
 RUNGWE